*Kioo cha Lugha, Juz. 20 (2), 165-183*
*Jarida la Taasisi ya Taaluma za Kiswahili*
*Chuo Kikuu cha Dar es Salaam* DOI: https://dx.doi.org/10.4314/kcl.v20i2.2

# Itikadi za Kisiasa katika Fasihi ya Watoto ya Kiswahili

*Faith M. Nyaga*[1]

**Ikisiri**

Hadithi katika vitabu vya fasihi ya watoto mara nyingi huwa fupi na vitabu hivyo huwa vidogo mno. Hali hii imechangia waandishi wengi kujiaminisha kwamba watoto wana akili ndogo na hivyo basi ni rahisi mno kuwaandikia vitabu (Fox, 1993). Fox anadai kwamba watoto huwa na uwezo mkubwa wa akili na hali hiyo huchangia katika ugumu wa kuwatungia hadithi. Anasema kwamba ni vigumu zaidi kutunga fasihi ya watoto kuliko fasihi inayolenga hadhira ya watu wazima. Lengo la makala hii ni kuonesha kwamba, humohumo katika usahili unaonuiwa kumnufaisha msomaji mtoto mna uchangamano katika kazi za fasihi ya Kiswahili ya watoto zinaposomwa kwa jicho kali la kiuhakiki kwa misingi ya kinadharia. Makala inakusudia kupambanua namna itikadi za kisiasa zinavyobainika katika fasihi ya watoto kwa kuchambua maudhui katika tungo hizo. Tungo zinazohakikiwa ni: *Usininyonye* (Komora, 1971), *Mkasa wa Shujaa Liyongo* (Matundura, 2001), *Karamu Mbinguni* (Kimunyi, 2002), *Zimwi la Leo!* (Wamitila, 2002) na *Sungura Mpanda Ngazi* (Kobia, 2008). Usampulishaji wa kimakusudi umetumika kuteua kazi hizi. Usomaji wa matini umeegemezwa katika Nadharia ya Umaksi. Je, tunaweza kupata fasiri tofauti inayohusiana na siasa mbali na ile wanayopata watoto wanapozisoma tungo hizi bila kutumia nadharia? Majibu ya swali hili yanapatikana katika makala hii.

## 1.0 Utangulizi

Fasihi ya watoto ni dhana inayorejelea fasihi inayolenga hadhira ya watoto. Fasihi hii kwa mujibu wa wataalamu kama Noun (2010), huchukua maumbo kiutanzu, kama vile ushairi, visakale, tamthilia na hadithi fupi. Matundura (2007) ameonesha kuwa fasihi ya watoto ni moja katika maeneo mbalimbali ulimwenguni. Sifa za

[1] Mhadhiri Msaidizi, Chuo Kikuu cha Chuka, Kenya. Baruapepe: fnyaga@chuka.ac.ke

kijumla[2] za kiulimwengu za fasihi ya watoto ni pamoja na ufantasia unaozipa mvuto wa pekee kwa lengo kuiteka saikolojia ya watoto. Wahusika katika kazi hizi mara nyingi husawiriwa kwa namna inayoonesha mapambano kati ya wema na waovu. Wahusika wanyama hupewa sifa za kibinadamu ili kuwavutia watoto. Sifa nyingine ya kilimwengu ya fasihi ya watoto ni ile ya matumizi picha au michoro. Picha au michoro ambayo huchukua sehemu kubwa kuliko matini, hutumiwa kimakusudi ili wasomaji (watoto) wasisahau kwa urahisi kile walichosoma. Michoro pia huwasaidia kuhusisha matukio katika hadithi na ulimwengu halisi.

Fasihi ya watoto, sawa na ilivyo fasihi inayolenga hadhira ya watu wazima, huakisi jamii katika ukamilifu wake kwa kufumbata masuala mengine zaidi kama vile siasa. Ingawa fasihi ya watoto huchukuliwa kuwa nyepesi na isiyoweza kusheheni masuala mazito ya kisiasa sawa na fasihi waliyoandikiwa watu wazima, makala hii inalenga kuonesha kwamba fasihi ya watoto ya Kiswahili husheheni itikadi za kisiasa. Kazi zinazohakikiwa katika makala hii ni: *Usininyonye* (Komora, 1971), *Mkasa wa Shujaa Liyongo* (Matundura, 2001), *Karamu Mbinguni* (Kimunyi, 2002), *Zimwi la Leo* (Wamitila, 2002) na *Sungura Mpanda Ngazi* (Kobia, 2008). Kazi hizi teule zilichapishwa katika vipindi mbalimbali baina ya miaka ya 1971 hadi 2008. Usomaji makini wa matini wa tungo hizi unaonesha mwingilianomatini wa namna fulani kuhusiana na suala la itikadi za kisiasa.

Ingawa watunzi wa kazi tunazozihakiki wametunga kazi nyingi za fasihi ya watoto, tumeteua tungo tunazozihakiki kimakusudi kwa sababu tunaamini zinasheheni itikadi[3] za kisiasa, hasa zinaposomwa kwa mkabala mwingine wa kihakiki usiokuwa wa ‘kitoto’. Kwa maneno mengine, makala inakusudia kuonesha kwamba, matini ya vitabu vinavyonuiwa kusomwa na watoto inaweza kusheheni masuala mazito sawa na fasihi dhati inayokusudiwa kusomwa na hadhira ya watu wazima. Kwa hivyo, matini hiyo inaafiki data ya makala hii.

---

[2] Hakuna kigezo kimoja kinachotosheleza uainishaji wa sifa za fasihi ya watoto. Matundura (2007) anaeleza kuwa kuna sifa za kijumla za fasihi ya watoto ambazo yaelekea zinakubalika ulimwenguni kote. Hadithi hizi huwa fupi na huandikwa kwa lugha na ploti sahili. Hadithi zilizoandikiwa watoto huegemea fantasia na huhusisha wahusika wa aina mbalimbali. Hadithi hizi hujishughulisha na maudhui ya kukua kwa watoto kwa lengo la kuwahamasisha watoto hao kuhusu masuala ya jamii, mienendo na uvumbuzi wa mambo mapya. Aghalabu, picha na michoro hutumika kwa wingi katika vitabu walivyoandikiwa watoto na mara nyingi hadithi nyingi huishia kwenye upeo wa furaha. Baadhi ya sifa hizi zilitumika katika utafiti huu kwa lengo la kubainisha jinsi itikadi za kisiasa zinavyobainika katika fasihi ya watoto ya Kiswahili kwa kuangazia maudhui, matumizi ya lugha, uhusika na wahusika.

[3] Hii ni mojawapo wa dhana ambazo ni ngumu kueleza. Kimsingi, tunaweza kusema kuwa itikadi ni mfumo wa mawazo fulani ambayo ni msingi na mwelekeo fulani wa kiuchumi au kisiasa. Kwa kawaida tunapozungumzia itikadi, huwa na maana ya mawazo ambayo yanachukuliwa au yanawahusu watu kadha hivi kwamba haihalisi kusema kuwa mtu fulani binafsi ana itikadi. Katika makala hii, dhana ya itikadi inamkutadhishwa na kuhusishwa na wahakiki wa zamani kama Karl Marx walioiangalia itikadi kwa mtazamo hasi – yaani wa mawazo danganyifu yanayotumiwa na tabaka linalotawala kuwapumbaza na kuwazuga waliotawaliwa.

**2.0 Itikadi na Itikadi za Kisiasa katika Fasihi**

Sutherland (1985) anadai kuwa hakuna fasihi isiyokuwa na hatia. Mtaalamu huyu anadai kwamba maadili yanayojenga hadithi huwa ni siasa za mwandishi na hata hatua ya mwandishi ya kuchapisha kitabu chake ili kisomwe na umma huwa ni kitendo cha kuonesha siasa. Hali hii inachangiwa na uhalisia kwamba imani na mitazamo yake husomwa na watu katika jamii hata na wale walio na mitazamo tofauti na mwandishi husika. Sutherland anaibua ushawishi wa aina tatu. Kwanza, anazungumzia kuhusu siasa za utetezi ambazo hujaribu kuonesha mtazamo wa mwandishi kuhusu ulimwengu kwa ujumla na jinsi anavyopendekeza mambo yawe au yanavyofaa kuwa kwa mtazamo wake ili kuathiri hisia za msomaji, fikra na tabia zake. Pili, ni siasa za kushambulia ambazo huibuliwa na mwandishi anapokumbana na jambo ambalo linakinzana na itikadi zake na yale anayoamini yanafaa kuwa, kama vile tabia chanya. Tatu, ni siasa za kuidhinisha ambazo huakisi mambo yalivyo katika jamii kwa kutilia mkazo maadili na mifumo ambayo tayari inaonekana na kukubalika na jamii fulani kwa ujumla.

Hoja za Sutherland (*keshatajwa*) ni muhimu katika makala hii kwa misingi kwamba inaangazia jinsi ambavyo waandishi wa kazi teule wamewasawiri wahusika ili kuibua maudhui yanayoendeleza, kukuza na kuakisi itikadi za kisiasa. Kwa mfano, wahusika vielelezo huwa wa kupigiwa mfano ili watoto wasomaji waathiriwe na hulka na matendo yao kwenye hadithi. Makala hii pia inaonesha jinsi wahusika waovu katika hadithi kwa kawaida wanavyokumbwa na mkosi katika maisha yao kama adhabu ya kufuata kaida tofauti na inayokubaliwa na jamii husika. Hapa waandishi waliibua haya kupitia maudhui, mbinu za lugha na usawiri wa wahusika.

Siasa za ushambulizi huwa si wazi katika kazi nyingi za fasihi ya watoto kama ilivyo katika kazi ilizotungiwa hadhira ya watu wazima. Sutherland (*keshatajwa*) anadai kuwa, waandishi wa fasihi ya watoto hukejeli watu waovu kwa lugha fiche lakini baadhi ya kazi walizoandikiwa watu wazima huweza kumkejeli mtu fulani katika jamii waziwazi. Akifafanua suala la itikadi, Hollindale (1988) anasema kwamba dhana hii katika fasihi ya watoto inaweza kuchunguzwa katika viwango vitatu. Kwanza, mwandishi huibua itikadi kupitia mambo anayoamini kuhusu jamii, siasa na maadili na hivyo basi hupendekeza mawazo yake kwa watoto kupitia hadithi. Kiwango cha pili huhusisha jinsi mwandishi anavyoyachukulia mambo ambayo hayajachunguzwa. Katika kiwango hiki, fasihi ya watoto huchukuliwa kama chemchemi ya habari ambayo hukusudiwa kufundisha na kupitisha maadili kutoka kizazi kimoja hadi kingine. Kiwango cha tatu ni kwamba itikadi huweza kudhihirika kila mahali. Nguvu za itikadi hudhibitiwa katika matini na huaminika kuwa huwa zinamzungukazunguka msomaji anaposoma hadithi fulani.

Kutokana na maoni ya Hollindale (*keshatajwa*), tunaweza kudai kwamba kila hadithi huwa na itikadi iliyofumbatwa katika imani na itikadi zinazochukuliwa kuwa za kawaida katika jamii. Simpson (1993) anafafanua dhana ya itikadi kama

mambo yaliyo katika jamii na ambayo yamepuuzwa lakini huwa yanatekelezwa na kuendelezwa na vikundi mbalimbali katika jamii. Fasihi ya watoto mara nyingi hupuuzwa na wahakiki kwa misingi kwamba ni ya 'kitoto' na kwamba haiwezi kusheheni masuala mazito ya jamii inamoibuka. Fasihi ya watoto hushughulikia maadili, mahusiano katika jamii, historia ya jamii inamoibuka na wakati mwingine hadithi huweza kudokeza matarajio ya baadaye ya jamii (Stephens, 1992).

## 3.0 Misingi ya Kinadharia

Usomaji wa matini za fasihi ya watoto ya Kiswahili zinazohakikiwa katika makala hii umeegemezwa katika Nadharia ya Umaksi, ambayo inahusishwa na mwanafalsa Karl Marx[4] na mwenzake Friedrich Engels[5] pamoja na wafuasi wao. Nadharia ya Umaksi hujishughulisha na mambo yenye uhalisia unaoonekana na mwanadamu kama vile uchumi, historia, jamii na mapinduzi. Kwa ujumla, Nadharia ya Umaksi ina mtazamo mzuri wa maisha kwa vile inajaribu kuwaeleza wasomaji asili ya mizozo inayopatikana duniani. Uwezo wa kiuchumi umepewa nafasi kubwa sana katika mataifa mengi duniani yanayopigania kuondoa utabaka miongoni mwao kama ukabila na ubaguzi wa rangi. Vipengele muhimu vinavyoweza kushughulikiwa katika fasihi kwa kulenga nadharia hii ni maudhui na wahusika.

Masuala yanayojitokeza katika tungo tunazozihakiki katika hadithi tunazozihakiki, kwa namna fulani, yanaweza kunasibishwa na Umaksi, kwamba kuna utajiri na faida inayopatikana kutokana na jasho au bidii ya wachache wanaohiniwa haki zao. Kwa ujumla, kilio cha wanyonge juu ya kukandamizwa kwa matumaini yao ya kujikomboa kutokana na ukatili wa watawala na watu wa tabaka la juu ni wazi katika kazi hizi teule. Waandishi wa tungo hizi wanafichua uovu wa mfumo wa kibepari. Kwa hiyo, Nadharia ya Umaksi inafaa kutumika katika kuchambua tungo teule ili kuonesha jinsi itikadi za kisiasa zinavyobainika katika fasihi ya watoto ya Kiswahili. Katika kuonesha muumano uliopo baina ya mwandishi, itikadi na Nadharia ya Umaksi, mhakiki Mwenda Mbatia (2001:24) anasema:

> Itikadi ya mwandishi haizuki katika ombwe tupu bali inatokana na mazingira mahsusi ya kiwakati. Dhana hii inahusishwa na Nadharia ya Umaksi ambapo inamaanisha mfumo wa kimawazo unaotawala katika kipindi, tabaka au jamii mahsusi. Baadhi ya waandishi wanaamini kuwa lazima msanii achague itikadi itakayomwongoza katika uandishi wake.

Kauli ya mhakiki huyu inakubalika, kwa msingi kwamba, Marx na Engels wanapambanua kuwa, historia ya binadamu huwa ni mapambano au harakati za kitabaka. Naye Wamitila (2003) anaeleza kuwa tabaka ambalo linadhibiti njia kuu

---

[4] Aliishi kati ya miaka 1818 na1883

[5] Aliishi kati ya miaka 1820 na 1895

za uzalishaji mali huitawala na kuidhibiti jamii. Marx anaeleza kuwa, jamii kielelezo inaweza kufikiwa tu ikiwa matabaka haya yataondolewa na uzalishaji pamoja na utumiaji kufuata misingi ya mahitaji. Marx alizumgumzia masuala yaliyohusu maendeleo ya jamii thabiti. Alieleza kuwa maendeleo ya jamii huthibitika katika vipindi vya maisha ambavyo kizazi cha binadamu kimepitia. Wafula (2006) anasema kuwa vidato ambavyo jamii inapaswa kupitia kabla ya kufikia ukamilifu wa kinjozi ni vifuatavyo: ujima, utumwa, umwinyi, ubepari, ujamaa na ukomunisti. Kulingana na maoni ya Marx, ukomiunisti ndicho kidato kikamilifu zaidi katika maendeleo ya binadamu. Kama ilivyo nadharia nyingine yoyote, Umaksi huwa na mihimili inayoipa nadharia hii mashiko. Mojawapo wa mihimili hiyo ni kwamba, historia ya maisha ya binadamu inaweza kuelezeka tu katika misingi yakinifu ya kiuchumi. Misingi hii inachunguza uzalishaji wa mali pamoja na miundo ya kiuchumi inayoathiri uzalishaji mali na usambazaji wake.

Njogu na Chimerah (1999) wanasema kuwa uchumi na siasa huingiliana. Hivyo basi, hatuwezi kuzungumzia siasa bila kurejelea uchumi wa eneo fulani. Kwa hiyo, Marx na Engels[6] wanasema kuwa daima historia ya binadamu itaakisi harakati zinazoendelea katika misingi yakinifu ya kiuchumi. Harakati hizi zinasababishwa na binadamu anayetafuta mahitaji ya kimsingi kama vile mavazi, chakula, makazi na usalama. Katika harakati hizi tabaka fulani la jamii hutoweka na jingine kuchipuka kwa sababu ya mgongano unaotokea kati ya tabaka tawala na tabaka tawaliwa.

### 4.0 Muhtasari wa Hadithi za ‘*Usininyonye*’ na ‘*Mkasa wa Shujaa Liyongo*’

*Usininyonye* (Komora, 1971) ni hadithi iliyoandikwa na Yuda Komora[7]. Hadithi hii inatumia istiari ya jamii ya himaya ya porini ambapo hapo mwanzo, wanyama, binadamu na viumbe wote wanaonekana kuwa marafiki wanaoishi pamoja kwa amani, umoja na udugu. Baadaye uhusiano baina yao unasambaratika kwa sababu ya unyonyaji unaoanzishwa na jamii ya kupe. Wanyama wengine wanajifungata masombo kuupinga unyonyaji huo. Mapinduzi haya yanafeli kwa sababu yanaongozwa na tamaa na ubinafsi wa wanyama. Unyonyaji huu unaendelezwa hadi nyumbani kwa binadamu ambaye ndiye mkuu wa viumbe vyote.

*Mkasa wa Shujaa Liyongo* (Matundura, 2001) ni hadithi ambayo imeandikwa na Bitugi Matundura[8]. Hadithi hii inahusu kinyang’anyiro cha

---

[7] Kazi nyingine za fasihi ya watoto ya Kiswahili za mwandishi huyu ni pamoja na *Sematongo na Hadithi Nyingine* (Longhorn, 2008), *Makombe Matupu na Hadithi Nyingine* (Longhorn, 2008), *Haguruka na Ningio na Hadithi Nyingine* (Longhorn, 2008) na *Mpopoo Nena Mpopoo Teka na Hadithi Nyingine* (Longhorn, 2008). Ingawa kazi hizi ziliandikwa zamani, mchapishaji alizitoa upya mnamo mwaka 2008.

[8] Tungo nyingine za fasihi ya watoto ya Kiswahili za mwandishi huyu ni pamoja na: *Mwepesi wa Kusahau* (Phoenix, 2005), *Masagisa na Zimwi Mbilikimo* (Phoenix, 2007), *Fahali Mtoboa Siri*

uongozi wa jimbo la Shanga kati ya Ndugu wawili, Liyongo na Daudi Mringwari. Baba yao Fumo anapofariki kutokana na ugonjwa, baraza la wazee linamteua Mringwari kurithi kiti cha ufalme cha babake. Miaka mitatu baada ya Mringwari kutawazwa mfalme, nduguye, Liyongo anatumia kila mbinu ili kujaribu kumwondoa kutoka mamlakani. Daudi Mringwari anahofia Liyongo atampokonya uongozi wake, na kwa hivyo anafanya njama ya kumwangamiza Liyongo. Kwa bahati nzuri, Liyongo anapata fununu kuhusu njama hizo na kutorokea Pate anakoenda kuishi na Wagalla. Mringwari anawatumia Wagalla ili wamuue Liyongo. Hata hivyo, Wagalla walishindwa kumkamata. Hatimaye, Liyongo anatiwa gerezani. Kupitia wimbo katika ngoma ya 'Gungu na Mwao'[9] Liyongo anamtuma kijakazi wao Sada kwa mamake Liyongo, ampelekee mkate wa wishwa wenye tupa ndani yake ili akereze minyororo na aweze kutoroka gerezani. Mfalme hakuiacha nia yake ya kumuua Liyongo hata baada ya Liyongo kufaulu kutoroka gerezani. Liyongo anasalitiwa na kuuawa na mwanawe, Moni.

### 4.1 Muhtasari wa *Karamu Mbinguni*, *Zimwi la Leo* na *Sungura Mpanda Ngazi*

Hadithi ya *Karamu Mbinguni* (Kimunyi, 2002) imeandikwa na Njiru Kimunyi[10]. Ndege wote wanapata mwaliko kutoka kwa Muumba wa kutalii mbinguni. Mwaliko huo unatokana na mienendo yao mizuri, wakilinganishwa na viumbe wengine duniani kama binadamu na wanyama. Katika kipindi cha wiki nzima ya matayarisho, Mungu anawapa uhuru na uwezo wa kubadili maumbile yao watakavyo ili wapendeze mbele yake. Baadhi yao, kwa mfano, Bundi wanatumia fursa hiyo kujibadilisha kwa nia mbaya ya kuwatisha ndege wengine. Mzee Kobe anawadanganya ndege kuwa alikuwa wa ukoo mmoja na ndege, kwani zamani Kobe walikuwa na mbawa kama ndege na viumbe wa mbinguni. Wanapofika mbinguni, ndege wanafurahia karamu waliyoandaliwa. Malaika anampongeza Mbayuwayu kwa kuwa mtiifu na kuwaadhibu Mbuni, Bundi na Kobe kwa makosa waliyoyafanya 'duniani'. Baada ya siku saba, ndege wanarudi duniani. Hadi leo, ndege wote huimba kwa furaha kila siku wakiusifu mwaliko wa karamu mbinguni, huku wakitumainia kuwa wataalikwa tena hivi karibuni.

Hadithi ya *Zimwi la Leo* (Wamitila, 2002) imeandikwa na Kyallo Wadi Wamitila[11]. Mwalimu wa kina Kelu na Kilo anawaambia wasimuliwe hadithi ya

---

(Focus, 2008), *Sitaki Iwe Siri* (Longhorn, 2008), *Adhabu ya Joka* (Longhorn, 2013), *Likizo ya Mkosi* (KLB, 2014), *Maadui wa Maria* (Vide Muwa, 2007), *Sifuri Nyani Mtalii* (Queenex, 2017), *Masaibu ya Mfalma Tapwara* (JKF, 2010), *Safari ya Maskauti* (Oxford, 2013) miongoni mwa nyingine.

[9] Ngoma mojawapo ya kizamani ya watu wa mwambao wa Afrika ya Mashariki.

[10] Kazi nyingine za mwandishi huyu zinazolenga hadhira ya watoto ni pamoja na *Nyumba ya Sungura*. Nairobi: Phoenix; *Mlima Kenya Kajifungua*. Nairobi: Phoenix Publishers Ltd; na *Mungu Nisaidie*. Nairobi: Phoenix Publishers Ltd.

[11] Mtunzi huyu ameandika katika takriban tanzu zote za fasihi. Vitabu vyake katika utanzu wa fasihi ya watoto ni pamoja *na Kadogo na Majini ya Nyanya*. Nairobi; Kenya Literature Bureau;

leo. Wanafunzi hawa wanashangaa, na Kelu anamwambia mwalimu wao kuwa hadithi zote ni za jana kwani zote huangazia matukio yaliyopita. Mwalimu wao anasisitiza kuwa inawezekana pia pakawa na hadithi ya leo. Hadithi ya *Zimwi la Leo* wanayosimuliwa na babu yao, Mzee Kanzi, inaangazia ukoloni na ukoloni mamboleo kwa njia fiche. Hadithi hii inalenga janibu za Afrika katika majilio ya mkoloni mkongwe na baadaye hatamu za uongozi zinapochukuliwa na Mwafrika ambaye anaendelea kumnyanyasa Mwafrika mwenzake. Kazi yoyote ya fasihi huangazia hali halisi katika jamii hasa jamii inayolengwa na mtunzi wa kazi hiyo. *Zimwi la Leo* inahusu mivutano ya kiuchumi na kisiasa katika katika enzi za ukoloni na baada ya uhuru. Hii ni hadithi ya kijazanda inayogusia masuala nyeti ya siasa na amali ya jamii kwa njia sahili. Inashughulikia ubepari na jinsi nchi za kigeni zinavyotawala nchi huru za Afrika.

*Sungura Mpanda Ngazi* (Kobia, 2008) ni kazi ya John Kobia[12]. Wanyama katika hadithi hii wanapokabiliwa na baa la njaa, wanawaza na kuwaza na kuwazua jinsi ya kujiepusha na bughudha hii. Sungura anaibua wazo la kuunda ngazi ili iwawezeshe kuyafikia maembe katika mwembe uliokuwa mrefu ajabu na wenye utelezi. Sungura anajitolea kupanda ili achume maembe na kuwarushia wanyama kutoka mwembeni. Wanyama wanajishughulisha kwa kila hali na kumsaidia Sungura kuuparaga mwembe. Anapofika juu ya mwembe, Sungura anakula maembe peke yake na kuwasahau wanyama waliomsaidia kuunda na kumpandisha mwembeni kwa ngazi. Wanateseka kwa njaa. Sungura anawadharau na kuanza kuwatusi wanyama wengine walio chini ya mti. Baada ya kusubiri kwa siku nyingi bila kupata kitu, wanyama wanakata tamaa. Wanyama wanakerwa na unafiki na usaliti wa Sungura na wanakata kauli kutafuta njia mwafaka ya kumwadhibu Sungura kwa kuwadhulumu. Wanaamua kuiondoa ngazi aliyoitumia Sungura kuukwea mwembe na kuivunjavunja kwa hasira. Sungura anasahau kwamba mpanda ngazi hushuka. Msimu wa maembe unapoisha, anagundua kwamba ngazi haipo, na wanyama wenzake wamekwenda zao kwa sababu ya hasira. Hana jingine ila kuruka kutoka kwenye mwembe, na hatua hiyo ina matatizo yake.

---

*Yatima*. Vide-Muwa Publishers Ltd. *Kijana Mpelelezi*. Vide-Muwa Publishers Ltd. *Jumba la Huzuni*. Vide-Muwa Publishers Ltd. *Msichana Mlemavu na Ndugu Zake*. Vide-Muwa Publishers Ltd.

[12] Mwandishi huyu pia amewatungia watoto kazi zifuatazo: *Tumbokarai* (JKF, 2008), *Usicheze na Nyembe* (JKF, 2008), *Fisi Mtunza Miti* (JKF, 2008), *Kusema Ukweli* (KLB, 2008), *Siku ya Ukimwi* (Longhorn, 2008), *Masalia* (Longhorn, 2008) na *Nikate Sikio* (JKF, 2009). Kazi nyingine ni pamoja na *Kiparangoto* (JKF, 2010), *Asiyesikia la Mkuu* (KLB, 2010), *Usiku wa Manane* (KLB, 2010), *Maskini Punda* (KLB, 2013), *Pembe za Mbwa* (KLB, 2014) na *Msitu wa Uma* (KLB, 2013).

## 5.0 Maudhui na Itikadi za Siasa katika tungo Hizi

Maudhui ni jumla ya mambo yote yanayozungumziwa katika kazi ya kifasihi. Maudhui hutumiwa kwa upana kujumlisha dhamira, falsafa, itikadi na msimamo wa mwandishi. Sehemu inayofuata inajadili maudhui na itikadi za siasa kutokana na tungo zilizotolewa kama ifuatavyo:

## 5.1 Ukoloni na Ukoloni Mamboleo

Ukoloni ulikuwa ni mfumo wa uongozi ambao ulizingatia kanuni ya kuyatawala mataifa mengine kisiasa, kiuchumi na kijamii. Ukoloni ulikuwa na nia ya kunyonya mataifa yaliyotawala. Mabeberu walilowea na kuanzisha himaya zao katika nchi za Afrika ili waweze kufikia malengo yao ya kiuchumi. Waafrika walinyang'anywa mashamba yao na kisha kuwa watumwa katika mashamba haya haya. Ubeberu ulidhihirika wakati wa ukoloni pale ambapo mali iliyozalishwa katika mataifa ya Kiafrika ilighurishwa na kupelekwa Ulaya. Watu wa tabaka[13] la juu wanafaidi jasho la wanyonge.

Katika *Zimwi la Leo*, kwa mfano, mwandishi anaonesha maingiliano ya siasa za kikoloni. Hadithi hii inaonesha awamu mbalimbali za historia kisiasa katika bara la Afrika. Awamu ya kwanza inaashiriwa na kuja kwa Zimwi[14] ambako kunaonesha jinsi wakoloni walivyoingia katika mataifa ya Afrika na kujidai kuwa wakarimu. Zimwi linawaahidi Wantu zawadi nyingi lakini lilikuwa na nia ya kufaidi jasho lao. Wakoloni wanajifanya kuwa walielewa maisha ya Waafrika na wanaonesha nia ya kuwakomboa kwa kuwa walichukulia kuwa Waafrika walikuwa wakiishi gizani. Zimwi linawapendekezea Wantu njia mpya za kulima likiwa na nia ya kuwanyonya.

Katika hadithi ya *Zimwi la Leo*, Wantu wanahadaika kwa haraka kwa tamaa ya kupata nguo nzuri na vitu vingine vizuri kutoka kwa Zimwi. Zimwi linafaulu kuwatumikisha Wantu katika mashamba makubwa na kujifaidi kutokana na jasho lao: Tunaambiwa:

> *Liliwaongoza watu hadi sehemu fulani palipokuwa na mashamba makubwa. Likawaonesha jinsi ya kulima. Nao wakaifanya kazi hiyo kwa bidii*[15]. Lile Zimwi liliendelea kula kila kitu. Lilipowaangalia wakishughulika kama nyuki kwenye mzinga wao lilisema kwa lugha ya ajabu, "Mmm…kuntu, vizuri! Mm…kuntu, vizuri sana. Mm…ntu…M…ntu." Jinsi Wantu walivyoendelea kufanya kazi,

[13] Hii ni dhana muhimu katika mikabala mbalimbali ya kiuhakiki hasa Umaksi, ambapo tabaka huelezwa katika misingi ya kiuchumi, kundi la watu ambao wana sifa sawa za kiuchumi huwekwa katika tabaka sawa.

[14] Mhusika Zimwi ametumiwa kijazanda kuwakilisha mkoloni na ukoloni.

[15] Maneno yaliyoandikwa kwa hatimlazo kwenye vifungu vyote vilivyodondolewa kutoka kwenye vitabu tunavyovihakiki yanaonesha msisitizo wetu.

> ndivyo Zimwi lilivyoendelea kula. Likaanza kunenepa (Wamitila, 2002:14-15).

Kipindi cha pili cha historia kinaoneshwa na juhudi za Waafrika kujikomboa kutokana na ukoloni mkongwe. Katika *Zimwi la Leo*, Wantu wanazinduka na kugundua kuwa uhusiano wao na Zimwi ni wa kuwanyanyasa. Mwandishi wa *Zimwi la Leo* anaonesha awamu ya tatu ya historia ambayo ni baada ya uhuru. Hata baada ya kuondoka kwa mkoloni mkongwe, ukoloni mamboleo unaendelezwa na viongozi wanaoshika hatamu za uongozi kutoka kwa Wazungu. Viongozi hawa waliiga kila mbinu ya utawala wa Wazungu na kuanza kuwanyanyasa Waafrika wenzao. Zimwi linapochoka kutawala, vizimwi vinachipuka ambavyo vinamsaidia kuendeleza uongozi wake. Vizimwi hivi vinaashiria ukoloni mamboleo. Tunaelezwa:

> Kulikuwa na sifa ya ajabu kuhusu ule mchezo wa kamari. *Kila aliyeshinda katika mchezo wa kamari alibadilika kwa sura na tabia.* Kiumbo alianza kuota mikono na vinywa vingi kama Bepari. Kitabia alianza kuwachukia wenzake polepole. Licha ya hayo, ile tamaa ya kuwa kama Bepari iliwanasa wote (Wamitila, 2002:29).

Waafrika wanakengeuka na kuiga mtindo wa utawala na utamaduni wa kigeni. Mabadiliko haya bado ni dhahiri katika nchi za Afrika. Athari za uongozi mbaya katika mataifa ya Afrika zimesababishwa na siasa na mfumo wa utawala wa ukoloni uliokuwapo.

Mwandishi wa *Usininyonye* anasawiri unyonyaji katika kipindi cha utawala wa mkoloni mkongwe na ukoloni mamboleo. Mtunzi anadhihirisha msimamo wake kwamba, afadhali ukoloni mkongwe kuliko ukoloni mamboleo kwani baada ya Mzungu kuondoka, Waafrika wanaona afadhali mkoloni mkongwe kwani Waafrika wenzao walioshika hatamu za uongozi waliwanyanyasa zaidi. Walinzi wa Mfalme Simba wanavunja sheria kwa kuwanyonya damu na kula nyama ya wanyama wenzao. Tunasoma:

> Basi huu ukawa ndio mtindo wa kila siku wa walinzi wa Mfalme Simba kufumaniwa wakivunja sheria kwa kuwanyonya damu na kula nyama za wenzao. Hatimaye, raia wake wote wakawa wanajihadhari wasikamatwe na wahalifu hao na wakapoteza damu na maisha yao pia. *Walikubali kuvumilia* kunyonywa *damu zao na kupe badala ya kuhatarisha maisha yao zaidi kwa kutafuta msaada kutokana na waliokuwa walinzi na askari wa Mfalme Simba. Maisha yao yalikuwa ya hatari zaidi kwa sababu tangu mbwa mwitu walipoonja damu na nyama walianza kuwafukuza na kuwaangamiza wanyama wote waliowaona* (Komora, 1971:14).

Kulingana na Marx, tabaka la jamii hutoweka na lingine huchipuka kwa sababu ya mgongano wa kitabaka. Mgongano huu hutokea kwa sababu kuna tabaka la wanyonyaji na wanaonyonywa. Katika hadithi ya *Usininyonye*, tunaelezwa kuwa wanyama waliona maisha yao yalikuwa ya hatari zaidi. Kadiri unyonyaji unavyozidi katika jamii, wanaowanyonya wengine huanza pia kunyonywa. Hata

Mfalme Kupe aliyekuwa mnyonyaji analalamikia unyonyaji wa Mfalme Simba na raia wake, anasema:

> *Sasa tumesikia na kushuhudia uchokozi mpya kutoka kwako na raia wako. Nyinyi pia mmeanza kunyonya damu. Sisi tukinyonya damu hubakisha akiba kwa siku zijazo. Lakini ninyi mkinyonya damu hampati raha mpaka mmalize kabisa na kula nyama na mifupa ya mnyama huyo.* Sasa sisi tumepatwa na shida ya njaa. Nami sina budi kutoa amri kwa raia wangu kunyonya damu zenu. Sasa hatutafanya ubaguzi wo wote. Wanyama wote watakipata cha mtema kuni! (Komora, 1971:15).

Hata baada ya kuondoka kwa mkoloni, athari zake bado zinaonekana. Licha ya nchi za Afrika kujipatia uhuru, bado Afrika inatawaliwa kupitia mlango wa nyuma. Katika hadithi ya *Zimwi la Leo*, tunaelezwa kuhusu uzembe na unene wa Bepari uliolifanya kushindwa kufanya lolote. Liliwategemea vizimwi kuendelea kulifanyia kazi yake ya kukagua kazi kwani liliviona kuwa na nguvu. Lilishindwa hadi kuoga na harufu ya jili lake ikaanza kutanda kila mahali. Harufu mbaya ya jili la Zimwi inawafanya Wantu kuanza kuliita Beberu kwani kila kitu kilikuwa kinanuka ubeberu.

**4.2 Uchaguzi wa Viongozi**

Siasa ni mhimili mmoja wa utamaduni wa nchi yoyote ile. Kila nchi hudhihirisha mfumo wa utawala ambapo viongozi hupewa vyeo na majukumu mbalimbali serikalini ili kurahisisha utawala wa nchi. Katika hadithi ya *Usininyonye*, kila taifa la wadudu, wanyama au ndege lilikuwa na mfalme wao. Kupe kwa mfano, alikuwa mkuu wa papasi, kunguni, chungu, siafu na chawa na alikuwa na jukumu la kutoa idhini ya serikali kwa wadudu wote.

Katika *Mkasa wa Shujaa Liyongo*, kuna wazee wa baraza katika Jimbo la Shanga wanaotumikia chini ya wafalme. Katika hadithi ya *Karamu Mbinguni*, Mbuni ndiye Malkia wa ndege wote duniani. Wote wako chini ya Muumba ambaye pia anasaidiwa katika utawala wake na Malaika. Wananchi wana jukumu na haki ya kumchagua kiongozi wao kupitia njia mbalimbali ikiwamo upigaji wa kura. Upigaji wa kura hunuiwa kuwakilisha maoni ya wananchi wengi. Katika hadithi ya *Sungura Mpanda Ngazi*, Sungura anawaambia wanyama kuwa alihitaji usaidizi wao ili aweze kuukwea mwembe kwani hangeweza kwa uwezo wake na umoja wao ulikuwa nguvu zao. Anaawambia:

> *Kama mjuavyo, siwezi kuukwea mwembe huu kwa uwezo wangu. Ninahitaji usaidizi wenu. Umoja wetu ni nguvu zetu. Kwa umoja wetu tutaweza kuyapata maembe yale. Nyinyi mnishikie ngazi, nami niipande*. Nikifika huko juu siwezi kamwe kuwasahau. Huwezi kusahau mkono unaokulisha. Kumbukeni ahadi ni deni (Kobia, 2008:9).

Katika uchaguzi wowote, kuna masharti na utaratibu wa kufuatwa hasa na watu wanaotaka kugombea nyadhifa mbalimbali serikalini. Katika hadithi ya *Mkasa wa Shujaa Liyongo* aliyefaa kuchaguliwa kama mfalme wa jimbo la Shanga, alihitajika kuwa amefikia umri wa makamo na atoke katika ukoo teule. Ukoo wa Fumo Liyongo, kwa mfano, unarejelewa kama ukoo teule, kwa hivyo, mfalme mpya angechaguliwa tu kutoka katika ukoo huo. Wakati mwingine, mapuuza na ujinga wa wananchi huwafanya kuwapendelea na kuwachagua viongozi wasiofaa na kuwapuuza viongozi walio na sifa na maarifa ya utawala. Haya yanaoneshwa katika hadithi ya *Karamu Mbinguni* ambapo baadhi ya ndege wanampuuza na kumdunisha Mbayuwayu kwa sababu yeye ni ndege mdogo. Hata hivyo, binamu yake, Jurawa anamuunga mkono na kumtaka awazungumzie ndege wengine. Baadaye, Mbayuwayu anadhihirisha uwezo wake anapofaulu kuwaongoza ndege hadi mbinguni bila matatizo yoyote.

Uchaguzi hufanywa ili kuteua kiongozi kwa njia ya haki. Katika jimbo la Shanga kwa mfano, wazee wa kijiji ndio walio na jukumu la kumteua mfalme mpya kwa kupiga kura ya maoni. Katika kisa cha *Mkasa wa Fumo Liyongo*, wengi wa wazee wa Shanga walipendelea Liyongo awe mfalme wao kwani:

> Baada ya Mzee Nabahani kuimaliza hotuba yake *kura ya maoni ilipigwa*. Wazee wengi walionekana kumuunga mkono Liyongo. Kulikuwa na sababu kadha wa kadha za kumpendelea Liyongo kama mfalme wao. Kwanza, *walimheshimu kwa kuwa mwepesi wa akili*. Pili alikuwa na *kipawa cha kuicheza ngoma aina ya 'gungu na mwao' walioiheshimu sana*. Juu ya hayo alikuwa na *mwili mnene wa kuheshimika*. Vilevile, *alikuwa na sifa ya kufanya kazi yake bila mchezo* (Matundura, 2001:20).

Ingawa wananchi hudaiwa kushirikishwa katika kuwachagua viongozi wao, kuna baadhi ya viongozi ambao hushika hatamu za uongozi kwa njia ya ulaghai. Tamaa ya kutaka kupata vyeo serikalini huwafanya baadhi ya viongozi kuwalaghai wananchi ili wapigiwe kura. Kwenye kisa cha *Karamu Mbinguni*, Kobe anapata fursa ya kuandamana na ndege kwenda kwa Muumba kwa kuwahadaa ndege kuwa asili yake ilikuwa imetokana na ukoo wa ndege na ule wa mbinguni. Kobe anamwambia Mbuni:

> Nilipata kuambiwa na mababu zangu ya kuwa mbinguni kuna raha tele. *Unionavyo mimi kwa hakika natokana na ukoo wa mbinguni. Ukiiangalia miguu yangu vizuri utaona ya kuwa ina maumbo yanayofanana na mabawa. Zama za zama sisi kobe tulikuwa na mabawa kama ninyi na viumbe wa mbinguni. Sisi na nyinyi tu wa ukoo mmoja*. Hakuna kiumbe mwingine katika dunia anayewakaribia kwa maumbile kama mimi. Viumbe wa mbinguni watafurahi sana kuniona tena huko baada ya mamia ya karne na karne za utengano. Mimi binafsi ningetaka kukutana na malaika. *Wananijua, wananitambua*. Tena usisahau ninaweza kusaidia sana katika safari hii (Kimunyi, 2002:31).

**5.2 Siasa za Unafiki na Nafasi ya Dini katika Siasa**

Nafasi ya dini katika utawala ni dhahiri katika nchi nyingi. Njogu na Chimera (1999) wanaeleza kuwa, ufuataji wa dini unaonekana kama njia inayoweza kumkomboa binadamu kutokana na tamaa, ufisadi, ubinafsi na matatizo mengi ya maisha yanayomkumba. Dini inakuwa suluhisho la maisha na inatoa mwangaza juu ya tabia zinazofaa kufuatwa. Katika hadithi ya *Karamu Mbinguni*, mhusika Mungu na Malaika wametumiwa kuwakilisha watu wa tabaka la juu na walio na uwezo kupita kiasi. Tunaelezwa pia kuwa, mbinguni kuna kwaya mbili, *ya Makerubi na Maserafi ambazo kazi yao ni kuimba na kumtukuza Mungu milele na milele* (uk. 42). Mwingiliano wa watu wa tabaka la juu na la chini ni nadra sana. Ingawa ndege walikuwa waende mbinguni, Mbayuwayu hana uhakika iwapo watakutana na Mungu. Tunaelezwa kuwa ndege wanapopata mwaliko wa mbinguni, wanajitayarisha na kujipamba kwa muda mrefu ili kumfurahisha Mungu. Mbayuwayu anawaambia ndege wengine:

> Nitawaongoza huko. Mwangojewa na malaika. *Labda mtapata nafsi ya kukutana na Mungu Muumba wetu. Sina hakika na hilo*. Lakini ningetaka kuwaambieni katika safari hii, jambo la muhimu liwe kutunza uhusino bora kati ya mbingu na dunia. *Tuanzishe uelewano wa kindugu kati ya ndege na malaika*… Kumbukeni ya kuwa siku zote za mbinguni ni sikukuu. Mimi mwenyewe nilikuwa kule kwa siku tatu. Niliyaona maajabu yasiyo kifani. Tunayo wiki moja ya matayarisho. *Tuitumie vizuri, ili tupendeze mbele ya Mungu wetu na Malaika wake* (Kimunyi, 2002:17).

Itikadi ya dini hutumiwa kama mbinu ya kuendeleza uongozi hata kama wakati mwingi dini hutumiwa kuonesha unafiki katika siasa. Viongozi wa kisisa huamini kuwa kuna kiumbe wa kipekee wanayeamini kuwa ana uwezo mkubwa kuliko wao. Katika hadithi ya *Mkasa wa Shujaa Liyongo*, Mzee Nabahani anawaonesha wazee umuhimu wa Mungu katika kuwaelekeza katika uteuzi wa kiongozi mpya. Anawaeleza:

> Mnajua kwamba hatuna mfalme wa kututawala…Mfalme wetu mpenzi Fumo alitutupa mkono. Ni wajibu sasa kuteua mmoja wa vijana wake kurithi kiti cha ufalme. *Hili ni jambo linalohitaji hekima kutoka kwa Mungu ili tuweze kufanya uteuzi wenye busara* (Matundura, 2001:18).

Baada ya hotuba yake, wazee wanakubaliana naye kwa kupiga makofi, kutikisa vichwa vyao na wengine kuvua kofia zao. Hii inaonesha kuwa kuna uhusiano mkubwa kati ya siasa na dini. Wazee wa jimbo la Shanga wanaamini kuwa ili wachague viongozi wazuri ni lazima waongozwe na Mungu.

Baadhi ya viongozi hujificha katika dini ili waweze kutekeleza maovu na kuendeleza uongozi mbaya. Dini katika uongozi hutumiwa kuwapumbaza wananchi ili waendelee kuunga mkono sera na uongozi ulio mamlakani. Unafiki huu wa dini unaoneshwa na ndege katika hadithi ya *Karamu Mbinguni*. Ingawa

ndege wana tamaa na nia yao ilikuwa kujinufaisha wakifika mbinguni, tunaelezwa kuwa walikuwa wanamtegemea Mungu kuwafikisha mbinguni salama.

### 5.4 Udikteta, Uongozi Mbaya na Vitisho

Kila Kiongozi huwa na mbinu ambazo hutumia ili kuhakikisha kuwa anaendelea kuongoza na kudumu uongozini. Nyingi ya mbinu hizi aghalabu huwa ni za kuwanyanyasa wananchi. Katika hadithi ya *Zimwi la Leo*, mhusika Zimwi ambaye ametumika kuwakilisha viongozi, amechorwa kama kiongozi anayezifahamu mbinu 'chafu' za kujiendeleza mamlakani hata kama hahudumii jamii ipasavyo. Zimwi linatumia ukali, vitisho, ahadi hewa, uongo, ulaghai na mauaji ili kuweza kuendeleza unyonyaji kwa Wantu. Linatumia ujanja mwingi ili kuhakikisha kuwa linaendelea kupata chakula kingi kutoka kwa Wantu. Uongozi wa kidikteta hutumia ukali na vitisho ili kuleta hofu miongoni mwa raia. Hili huwafanya kuhofia kujikomboa na huwasababisha watu kuwatumikia viongozi kama watumwa. Zimwi liliwaogofya wahusika Wantu kwa sababu ya makono yake mengi yenye nguvu nyingi. Liliwalazimisha kulipa kodi ya kuishi huku likiwaangalia kwa mtazamo mkali wa macho mekundu kama damu. Tunaelezwa:

> Kimya cha muda kilipita huku Kabaila likiwaangalia kwa mtazamo mkali wa macho mekundu kama damu. *Yale macho yaliwatia Wantu hofu na woga mwingi. Ndimi nyingi za Kabaila zilitokeza kama miale ya moto na kuwatisha*. "*Kila mtu lazima atoe kodi*. *Atakayekataa tutapambana*." Lilinguruma kama radi. **"**Nimejua! Nitawaambia kuwa lazima walipe kodi! *Yule ambaye hatalipa nitapambana naye; atakiona cha mtema kuni*" (Wamitila, 2002:20).

Zimwi linawalazimisha Wantu kushirikiana nalo na waliotaka kukaidi amri na masharti ya Zimwi wanatishwa kwa kuambiwa kuwa lazima walipe kodi. Zimwi linawaza jinsi ya kuendelea kuwanyonya Wantu na linaibuka na njia ya wao kulipa kodi. Hii ilikuwa njia ya kuwanyang'anya mapato yao. Wantu wanaendelea kuwa maskini huku Zimwi likitajirika.

Viongozi wa kisiasa hutumia kila mbinu kuwanyamazisha wapinzani wao na kuteteresha nguvu za ukombozi. Propaganda ni mbinu maridhawa zinazotumiwa na tabaka tawala kuhifadhi na kuendeleza nafasi yake. Katika hadithi ya *Mkasa wa Shujaa Liyongo*, wazee wanapoalikwa katika mkutano kwenye ukumbi wa Mfalme ili kuchagua mfalme mpya, hawakujua walichoitiwa lakini walikuwa wameanza kueneza propaganda kuwa ukoo wa Fumo ulitaka kunyang'anywa uongozi. Tunaelezwa:

> Wazee hawakujua kwa uhakika walichokuwa wakiitiwa. Walilojua tu ni kwamba lazima kulikuwa na jambo zito. Wengine walifikiria kuwa kungekuwa na sherehe ya kumbukumbu ya kifo cha mfalme. Wengine walifikiria pengine kulikuwa na vurugu na vurumai baina ya wajane wa Fumo. *Wengine hata walinong'onezana kuwa baraza lilitaka*

> *kupitisha hoja ya kuutwaa uongozi kutoka kwa ukoo wa Fumo*! (*Mkasa wa Shujaa Liyongo,* 2001:15).

Mnong'ono huu unaashiria kuwa, hata kama uongozi unaweza kupitishwa kwa watu fulani tu katika jamii, siyo kila mwananchi huridhika na utawala ulioko. Liyongo pia alitumia propaganda nyingi ili kuharibu sifa za utawala wa Mfalme Mringwari kwani baadhi ya wananchi akiwamo Liyongo hakumtaka Mringwari kama kiongozi wao.

Pindi hila zingine za Mfalme Mringwari zinaposhindwa kumuua Liyongo, hofu na vitisho vinakuwa silaha zingine anazotumia. Katika utawala wa kidikteta, vitisho huwa ni mbinu ya kuwanyamazisha watu wanaopigania haki zao na wale wanaopinga sera za utawala wa serikali. Liyongo aliamini kuwa kiti alichokalia Mringwari kilikuwa chake (Liyongo) kwa haki. Juhudi za Liyongo kupata haki yake ya kuwa Mfalme wa Shanga zinagonga mwamba kwani Mringwari anamtisha na kumwambia:

> Wazee waliniteua mimi. Wewe ni nani kuupinga utawala wangu? Sharti ukumbuke kwamba mimi nina jeshi langu linalonitumikia. *Ikiwa utaendelea kuwa* na *kichwa kigumu na kunionesha ujeuri basi sina budi kukuhakikishia kwamba unathubutu kucheza na moto*. Nachukua fursa hii kukuonya mapema unikome. *Unikome kama ulivyolikoma titi la mama yako!* (Matundura, 2001:27).

Mringwari alijua kuwa watu wa Shanga walimpenda Liyongo na hivyo alikuwa anatafuta njia na namna za kumnyamazisha Liyongo. Mfalme Mringwari alijua kuwa ufalme wake ulikuwa hatarini na Liyongo angewachochea watu ili kumwondoa mamlakani. Mringwari anamtisha Liyongo na hata kumkumbusha kuwa jeshi lake lingemchukulia hatua angeleta fujo katika jimbo la Shanga.

Viongozi wanaoendeleza mfumo wa kimabavu kutawala, hawawashirikishi wananchi katika maamuzi yoyote na hawakubali kukosolewa na wananchi kwa lolote. Katika hadithi ya *Usininyonye*, Jemedari Chui anapendekeza wazo la kuwasaidia wanyama wenzao kuwang'oa kupe waliowanyonya ili afaidi. Wakili Sungura anapojaribu kumkosoa Jemedari Chui aliyekuwa mmoja wa viongozi, tunaelezwa kuwa wanawanyamazisha sungura wote na kuwafukuzia porini. Sungura anaona si vyema kwa wanyama kuwadonoa wenzao kupe kwani wakionja damu yao, watakuwa na hamu ya kuendelea kunyonya damu na unyonyaji ungeendelea badala ya kukomeshwa. Babu Ndovu na wafuasi wake hawakufurahishwa na maoni haya ya Sungura. Babu Ndovu anasema:

> "Nani huyo mjinga? *Nyamaza!* Nenda zako na kupe waendelee kukunyonya kama hivyo ndivyo upendavyo."…wakaendelea wote huku *wakiwarukia sungura wote ili wawafukuze*. Basi *sungura wote wakafukuzwa* kutoka *mkutanoni huo*. "Usiyafikirie maneno machafu ya Sungura, ewe mfalme mtukufu. Sisi tumeona maneno ya busara ya Jemedari wako mkuu yatutosha. Nasi tuko tayari kuanza kufanya hivyo tangu leo. Twaweza kuanza sasa hivi kama watu wako wako tayari,"

> akasema Punda Milia…na mkutano wote ukaitikia kwa kauli moja wakikubaliana naye (Komora, 1971:10).

Viongozi wana jukumu la kuwa kielelezo bora katika jamii. Mwandishi wa hadithi ya *Usininyonye* anaonesha umuhimu wa viongozi katika kupinga itikadi hasi za kisiasa katika jamii kama vile unyonyaji. Viongozi wasiozingatia uadilifu katika jamii huweza kuathiri nchi na watu kwa njia mbaya. Viongozi walioshikilia nyadhifa mbalimbali katika jumuiya ya *Usininyonye* ndio wanaoanzisha na kuendeleza unyonyaji.

Kwa mfano, Babu Ndovu anamlaumu Mfalme Kupe aliyekuwa mfalme wa wadudu kwa maasi yake akisema:

> Zamani tulikuwa na nguvu miilini mwetu. Hatukusikia maumivu yo yote. Hakuna kazi iliyotushinda. Mbio ilikuwa mchezo wetu. Lakini tangu kupe, papasi, chawa na siafu waanze kutushambulia, hatuna nguvu miilini mwetu. Hatuna raha yoyote; twasikia maumivu tu. *Haya yote ni matokeo ya maasi ya Mfalme Kupe. Kama mwenda wazimu yule hangeanza ubaradhuli wake wa kula damu yetu, maafa haya hayangalitupata* (Komora, 1971:21).

Kaka Nyati pia anakubaliana na Babu Ndovu kwa kusema kuwa hasara yote ya unyonyaji waliopata haingepatikana kama Mfalme Kupe asingeanza ulafi wake. Mfalme Kupe aliwachochea kupe wenzake ili wazidi kuwanyanyasa wanyama kwa kuwanyonya damu. Kama kiongozi, Mfalme Kupe alifaa kuwaongoza wadudu waliokuwa chini yake kukomesha unyonyaji.

Unyonyaji ulipokithiri porini, kila mnyama, mkubwa kwa mdogo, anaathirika na kuanza kujutia tabia hii ya unyonyaji miongoni mwao. Katika hadithi ya *Usininyonye*, Babu Ndovu anajuta kwa sababu ya unyonyaji na anamwambia kaka Nyati kuwa anadhani maisha ya zamani yalikuwa mazuri kuliko ya wakati huo. Anakumbuka jinsi maisha ya zamani yalivyokuwa na amani na mazuri na hawakuhangaika sana kwani hakukuwa na unyonyaji. Anakumbuka kuwa hawakuwa na vifo vingi, hofu, woga na magonjwa. Mwandishi anatumia madhara ya unyonyaji na majuto kama njia ya kupendekezea wasomaji kuwa na siasa zisizo na unyonyaji katika jamii.

### 5.5 Uzalishaji Mali na Ubinafsi

Umaksi huhusisha itikadi na uzalishaji mali na jukumu lake katika mivutano ya kisiasa katika jamii. Umaksi pia huchukulia kwamba jamii zote za kitabaka huzalisha mkururo wa miundo ya urazini inayokinzana na kushindana. Urazini wa mwanadamu umeundwa na itikadi. Hivyo, mwanadamu huuona ulimwengu wake na huelezea yale yaliyomzunguka na yale anayoyaona kuwa kweli kupitia imani, thamani ya kitu na namna yake ya kufikiri na kuhisi. Matabaka yaliyo katika jamii huwa na mitazamo na maoni tofautitofauti kuhusu maisha.

Umaksi unashikilia kwamba, kitu cha msingi katika maisha ya binadamu ni mahitaji ya kimsingi. Hivyo, jambo la kwanza ambalo binadamu hushughulika

nalo ni kutafuta njia ya kukidhi mahitaji haya ya kimsingi: kula, kunywa, kupata malazi na mavazi. Ili aweze kutimiza mahitaji haya, binadamu hujiunga pamoja, aghalabu katika makundi ili aweze kuzalisha mali kwa wepesi. Binadamu hugawa kazi na majukumu mbalimbali katika makundi haya. Makundi haya ndio husababisha kuchipuka kwa matabaka katika jamii. Watu hutengana na kuzuka tabaka la juu, la kati na lile la chini. Katika hadithi ya *Zimwi la Leo*, inaelezwa:

> Wengine walijaribu kuungana na kuukataa mchezo wa kamari. *Walioshinda waliendelea kujitenga na wenzao na kulipenda Bepari zaidi*. Utengano mkubwa ulianza kuingia baina yao. *Kundi moja la Wantu lilichukia Bepari lakini jingine liliendelea kulipenda*. Bepari halikujali kwa kuwa lilikuwa bado na uwezo mkubwa. *Liliendelea kunenepa na kujenga miji mingine kutokana na juhudi na nguvu za Wantu. Baadhi ya miji liliwakabidhi* waliofanana *nalo* (Wamitila, 2002:30).

Hatua ya juu ya mwendelezo huu ni uzukaji wa mfumo wa ubepari. Mfumo huu wa kibepari huzuka pale ambapo mgawanyiko huu wa kitabaka unaendelea. Katika mfumo huu, mali humilikiwa na watu wachache ambao hupata mali yao kutokana na unyonyaji wa umma na hasa wafanyakazi. Zimwi linafakamia mapato ya Wantu na kuwa tajiri.

Katika jamii zilizo na matabaka, unyonyaji na dhuluma ni dhahiri. Wanaotia bidii ili kujinufaisha hawafaidiki na jasho lao. Watu wa tabaka la chini ndio hutumiwa kuzalisha mali katika nchi na mapato yake kufaidi watu wa tabaka la juu. Tabaka la juu huwanyima haki walio katika tabaka la chini ila tu kuwanyonya jasho lao. Suala la unyonyaji linawekwa wazi katika hadithi ya *Sungura Mpanda Ngazi.* Fisi anawakemea wanyama wengine kwa kumcheka anapoyakosa maembe mabivu:

> Mbona nyinyi mnanicheka? Maembe yakianguka yatakuwa mali yetu. Wengi wenu wanaocheka ndio watakaokuwa wa kwanza kukimbilia maembe yakianguka (Kobia, 2008:3).

Matabaka katika jamii huwa na haja tofauti kutegemea tabaka lao na kinachozuka ni mikinzano kuhusu mapato na nguvu za kutenda kazi. Jinsi watu katika matabaka husika wanavyoelewa msingi wa maisha yao hutokea kuwa kamba ya mvutano ambapo wanaweza ama kubadilika au kuendelezwa. Mhusika Fisi anajua fika kwamba, licha ya yeye kujibiidisha kuangusha maembe, kila mnyama atataka kupata maembe mabivu yatakapoanguka. Haya yanadhihirisha kuwa watu wanaozalisha mali, hawafurahii matokeo ya juhudi zao na badala yake wengine ndio hufaidika.

**5.6 Siasa za Kikabila na Utabaka**

Kila nchi huwa imegawika katika himaya mbalimbali ambazo aghalabu hugawanyika kwa misingi ya kisiasa na sababu za kiutawala. Hadithi ya *Karamu Mbinguni* inaangazia himaya mbili ambazo ni mbinguni ambayo ina viumbe wa mbinguni na himaya ya duniani iliyo na ndege, wanyama na binadamu. Mwandishi anasawiri himaya ya mbinguni kama yenye nguvu na ya kipekee kwani ni nadra

kwa wanyama wengine kwenda huko. Ndege wanashangaa wanaposikia kuwa Mbayuwayu alikuwa mbinguni kwa Muumba wao na alikuwa ametumwa salamu kwa ndege wote. Tunaelezwa:

> Ndege walishangaa. Walimwangalia Mbayuwayu. Hawakuamini maneno yake. Kanga alisema hata bila ya kuomba ruhusa kutoka kwa Malkia Mbuni, "Mbayuwayu ikiwa katika nyendo zako nyingi umerukwa na kichwa, twakuomba ukae upumzike. Una wazimu wewe? *Tangu lini kiumbe yeyote akawahi kufika mbinguni?*" (Kimunyi, 2002:11).

Utangamano wa Mhusika Mbayuwayu na watu wa mbinguni unawashtua ndege kwa kuwa ni nadra kupata watu wa tabaka la chini wakihusiana vyema na watu wa tabaka la juu. Wahusika wanaishi katika himaya zao na huweza kutembea katika himaya nyingine kwa mwaliko tu. Mbuni anamwambia Mzee Kobe kuwa walikuwa na karamu mbinguni kwani walikuwa wamepata mwaliko rasmi. Katika himaya hizi, kuna makundi mengine ambayo huhusisha jamii mbalimbali. Hadithi ya *Karamu Mbinguni* inaonesha kuwapo kwa makabila mbalimbali katika himaya husika. Duniani, kwa mfano, pana ndege na wanyama na katika kundi la ndege pana makundi mengine tofautitofauti ya ndege. Makundi haya yanaweza kutumiwa kuwakilisha makabila mbalimbali ya nchi.

Watu katika jamii hujigawa katika makundi mbalimbali yasiyo na usawa. Aghalabu, makundi haya hutegemea uwezo wa watu wa kiuchumi. Siasa za kikabila na utaifa pia huweza kutumiwa kama kigezo cha kugawa watu katika matabaka mbalimbali. Jamii za kabila moja huweza kudhihirisha umoja wao kwani hujichukulia kama watu wa aila moja. Kuna jamii za watu wachache na jamii zingine huwa na watu wengi. Katika hadithi ya *Karamu Mbinguni*, ndege wanapata mwaliko wa kwenda mbinguni. Mbayuwayu anawaeleza:

> "Mungu Muumba wetu akasema ya kuwa tunao uhuru wa uwezo wa kujibadili tutakavyo. Akaongeza kuwa tukiliomba lolote litatokea. Kwa hivyo, kila mmoja wetu ajipambe vizuri. Kabla ya kwenda tutakutana hapa ili tuyarekebishe makosa yakiwepo. Kwa sasa tuna siku tano za matayarisho. Tuzitumie siku zenyewe vizuri. Nendeni mkajitayarishe." *Ndege waliondoka mmojammoja. Wengine kama Korongo walikwenda kwa makundi. Zao zilikuwa ni jamii kubwa* (Kimunyi, 2002:19).

Korongo wanatembea katika makundi kwa sababu ni wengi. Korongo katika hadithi hii wametumika kuwakilisha watu wa kabila moja ambao wana idadi kubwa katika nchi. Kwa kawaida, kabila lenye watu wengi huonekana kuwa na uwezo na ushawishi mkubwa wa kisiasa. Sababu ni kwamba, siasa za kikabila huendelezwa katika jamii na huwafanya wananchi kuwachagua viongozi kwa misingi ya kikabila. Hili huchangia kuwapo na viongozi wengi katika kabila moja na upendeleo huonekana hasa katika uteuzi wa watu kutoka kabila hilo katika vyeo na nafasi mbalimbali serikalini.

Ukabila hutumiwa na watu wenye ubinafsi kuwahini wenzao fursa ya kustawisha maisha yao. Katika hadithi ya *Usininyonye*, familia ya Bwana Moto inamtegemea ili awape nguo, chakula na karo kwa misingi kuwa alikuwa ameelimishwa na wazazi wake na kuwa mwalimu. Babake Bwana Moto kupitia barua yake kwa Moto anamwambia:

> *Wewe siku hizi umenisahau*. Huniletei nguo wala chakula. Mama yako, dada zako na ndugu zako pia hawana chakula wala nguo. Watoto wa ndugu yako hawakwenda shuleni kwa ukosefu wa karo. Wewe umeacha wajibu wako wa kuwatunza wazazi wako. *Ikiwa mtoto hawezi kuwatunza wazazi wake, ni faida gani ya kuzaa au kuzaliwa? Ikiwa huwezi kuwasaidia ndugu zako na watoto wao pia wapate elimu, basi faida ya kuwa ndugu, kaka, mjomba, baba mdogo, au baba mkubwa wao ni ipi? Radhi yangu na ya babu zako* utaipataje ikiwa tabia yako ni hii? (Komora, 1971:35).

Yuda Komora, mtunzi wa *Usininyonye* anaonekana kupinga siasa za ukabila na upendeleo katika jamii kwani tunamuona mhusika Bwana Moto akikataa kutwikwa mzigo wa kusaidia familia yake na kusema kuwa hawezi kuwapa watu vitu vya bure hata kama ni wa damu moja. Babake Bwana Moto hata anamlaghai kwa kumtisha kuwa asiposaidia watu wa aila yake hangepata radhi yake na ya babu zake. Mwandishi anaonesha hii kuwa aina fulani ya unyonyaji katika jamii.

## 6.0 Hitimisho

Lengo la makala hii lilikuwa kuonesha kwamba, fasihi ya watoto, licha ya usahili wake, inaweza kusheheni maudhui mazito kuhusu itikadi za kisiasa. Mifano kutoka vitabu vya fasihi ya watoto tulivyoviteua kimakusudi, imeonesha kwamba humohumo katika usahili wa fasihi ya Kiswahili ya watoto, mna uchangamano wa kimaudhui. Watoto huenda wasizifasiri kazi hizi kwa namna ambavyo tumezifasiri au kuzipokea kwa mwitiko wa aina hii kwa sababu ya umri wao na kutokuwa na tajiriba za nadharia.

## Marejeleo

Chimerah, R. na Njogu, K. (1999). *Ufundishaji wa Fasihi: Nadharia na Mbinu*. Nairobi: Jomo Kenyatta Foundation.

Fox, M. (1993). “Men who Weep, Boys Who Dance: The Gender Agenda Between the Lines in Children’s Literature.” *Langage Arts.* Kur. 84-88.

Kimunyi, N. (2002). *Karamu Mbinguni*. Nairobi: Phoenix Publishers.

Knowles, M. na Malmkjær, K. (1996). *Language and Control in Children's Literature*. London/New York: Routledge.

Kobia, J. (2008). *Sungura Mpanda Ngazi.* Nairobi: KLB.

Komora, Y. (1971). *Usininyonye*. Nairobi: Longhorn Publishers.

Marx, K. na Engels, F. (1971) *The German Ideology*: *Literary Theory* Oxford: Blackwell Publishers.

Matundura, B. (2001). *Mkasa wa Shujaa Liyongo*. Nairobi: Phoenix Publishers.

Matundura, B. (2007). Taswira Dumifu za Uana katika Fasihi ya Kiswahili ya Watoto. Tasnifu ya Umahiri (Haijachapishwa). Chuo Kikuu cha Nairobi.

Mwenda, M. (2001). *Kamusi ya Fasihi*. Nairobi: Standard Textbooks Graphics.

Nyaga, F.M. (2017). Itikadi za Kisiasa katika Fasihi ya Kiswahili ya Watoto. Tasnifu ya Umahiri (Haijachapishwa). Chuo Kikuu cha Chuka.

Ngugi, P. (2009). Language and Literary Education: The State of Children's Literature in Kiswahili in Primary Schools in Kenya. Tasnifu ya Uzamivu (Haijachapishwa). University of Wien.

Njoroge, N. (1978). "African Oral Literature: Fighting Literature." Katika E. Gachukia na A. Kichamu (Wah.), *Teaching of African Literature in Schools.* Nairobi: Kenya Literature Bureau.

Nkata, D. (2001). "Continuity and Change in Storytelling: Children's Stories in Uganda's Past and Present." Paper presented at the 15th IRSCC Biennial Conference: Warmbatha, South Africa.

National Open University of Nigeria (NOUN) (2010). *Children's Literature*. Lagos: National Open University of Nigeria.

Osazee, F.P. (2004). "Not only Books for Africa but A Reading Culture Too." Keynote Address presented at the 29th IBBY Congress. Cape Town. South Africa. 5-9th Sept.

Simpson, P. (1993). *Language, Ideology and Point of View.* London: Routledge.

Stephens, J. (1992). *Language and Ideology in Children's Fiction.* New York: Longman.

Stephens, J. na Watson, K. (Wah.). (1994). *From Picture Book to Literary Theory*. Sydney: St. Clair Press.

Sutherland, R. (1985). "Hidden Persuaders: Political Ideologies in Literature for Children." *Children's Literature in Education*. Juz. 16(3): 143-157.

Wafula, R. (2006). *Nadharia za Uhakiki wa Fasihi.* Nairobi: JKF.

Wamitila, K.W. (2002). *Zimwi la Leo*. Nairobi: Longhorn Publishers.

Wamitila, K.W. (2003). *Kamusi ya Fasihi. Istilahi na Nadharia.* Nairobi: Focus Publications Ltd.

Wamitila, K.W. (2003). *Kichocheo cha Fasihi: Simulizi na Andishi.* Nairobi: Focus Publications Ltd.